Umoja wa Mungu
MWONGOZO YA KUJIFUNZA

DAVID K. BERNARD &
Neil Stegall

Soma la 1
Uimani wa Mungu Mmoja wa Wakristo

A. Maelezo
   1. Uimani wa Umoja wa Mungu: imani katika Mungu Mmoja.
   2. Atheisim: kukataa kuwepo kwake Mungu.
   3. Agnosticism: Imani kwamba kuwako kwa Mungu hakujulikani au labda hajulikani.
   4. Pantheisim: uimani kuwa Mungu ni asili au jeshi la ulimwengu.
   5. Polytheisim: uimani wa zaidi ya Mungu Mmoja.
      a. Ditheisim: uimani ya miungu wawili
      b. Trithesim: uimani wa miungu watatu
   6. Uimani Mbali Mbali za Ukristo.
      a. Utatu: uimani wa kuweko kwa nafsi tatu “katika” uungu
      b. Binitarisim: uimani wa nafsi mbili
      c. Umoja wa Mungu halisi (ikiengua wingi wa nafsi) pamoja na kukataa uungu kamili wa Yesu Kristo. Mifano Arianisim, na elimu inayoendesha mornochianisim.
      d. Umoja wa Mungu halisi: (ikiengua wingi wa nafsi) na kuthibitisha uungu kamili wa Yesu Kristo. Mifano Modalistic (uimani wa umoja wa Mungu); Umoja wa Mungu.

B. Misisitizo ya Agano la Kale
   1. Kumbukumbu la Torati 6:4 linafundisha umoja wa Mungu kabisa.
      a. Ni ukiri wa imani ya Kiyahudi kihistoria unaoitwa Shema.
      b. Ni muhimu daima kufundisha (Kumbukumbu 6:5-9).
      c. Ni amri ya kwanza iliyo kuu zaidi (Marko 12:28-31).
   2. Mungu alitangaza umoja Wake pekee katika Isaya: “Mimi ni Bwana, wala hapana Mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu….” (Angalia Isaya 37:16; 42:8; 43:10-11; 44:6, 8, 24; 45:5, 6, 21-23; 46:5, 9; 52:6.)
   3. Zaidi ya mara hamsini katika Biblia Mungu huitwa “mtakatifu mmoja” walakini kamwe siyo wawili au watatu watakatifu. (Tazama Isaya 54:5.)
   4. Watakatifu wa Agano la Kale hawakuwa na wazo la kiutatu.

C. Msisitizo wa Agano Jipya.
   1. Linathibitisha umoja wa Mungu (Warumi 3:30; Wagalatia 3:20; 1 Wakorintho 8:4, 6; Yakobo 2:19).
   2. Kuna Mungu Mmoja tu na mpatanishi mmoja (Yohana 17:3; 1 Timotheo 2:5).
      a. Mpatanishi ni yule asiye na dhambi Yesu, katika yeye Mungu alidhihirishwa. Alipatanisha Mungu mwenye haki na wanadamu wenye dhambi.
      b. Kama ilikuwepo nafsi ya pili iliyo na ulinganifu, asingeweza kuwa mpatanishi; pia angelihitaji mtu kumpatanisha yeye na uanadamu wenye dhambi.
   3. Yesu aliwathibitishia wazo la Wayahudi la Mungu (Marko 12:29; Yohana 4:22).

Andiko la Kukariri: Kumbukumbu la Torati 6:4; 1 Timotheo 2:5
Ufafanuzi: Monotheisim, atheisim, agnostisim, pantheisim, polytheisim, thritheisim, trinitirianisim, Shema.

Soma la 2
Hali ya Mungu (Mungu ni Nani)

A. Mungu hana hali za Tabia za asili
   1. Uzima
   2. Wa pekee
   3. Ajielezaye katika hali yake.
   4. Kiroho (Yohana 4:23-4)
      a. Siyo hali ya vitu; siyo mwili, damu, mifupa
      b. Halinganishwi na mwili
      c. Tangu kufanyika mwili, Mungu amefunuliwa kikamilifu kuwa ni Yesu; hakuna Mungu anayeonekana mbali ya Yeye (Yesu)
   5. Asiyeonekana (Yohana 1:18; 1 Timotheo 3:16)
   6. Wa Pekee aliyepo
   7. Wa milele
   8. Asiyeonekana (mahali pote yupo) (Zaburi 139). Maelezo ya Mungu kuwa mbinguni yanaonyesha haya (a) Mungu hafungwi na tunavyofikiri/hafungwi na mahali fulani hapa duniani; (b) Hutuonyesha mahali pa Mungu penye hoja na shughuli Zake ("makao makuu"); (c) Hutaja mahali pa Mungu, ambako kumejaa utukufu na mamlaka Yake; (d) Inawezekana Biblia inaonyesha mahali pake Mungu anapojidhihirisha na malaika Zake.
   9. Anajua yote
   10. Mwenye uwezo wote
   11. Asiyebadilika (hali ya kutokubadilika)
   12. Upeo wa hali ya juu (zaidi ya mwanadamu awezavyo kutambua, isipokuwa kwa ufunuo)

B. Hali za Kimaadili
   1. Mtakatifu
   2. Haki na Mnyofu
   3. Upendo
   4. Rehema na Neema
   5. Uaminifu
   6. Mkweli
   7. Wema

C. Anthropomorphisim – Elimu ya kumwelezea Mungu bila pasipo:
   1. Maelezo ya kutokuwa mwanadamu (Mungu) katika maneno ya kibinadamu (kwa ajili ya uelewevu wazi wa kuelewa kwetu)
   2. Hasa, usemi wa Mungu kuwa na macho, mikono, moyo, miguu, pua na kadhalika.
   3. Maelezo haya ni mifano, fikira; kwa mfano "miguu" ya Mungu siyo halisi kwamba iko juu ya dunia.

D. Tendo la Kuonekana kwake Mungu (Theophanies)
   1. Maelezo: Udhihirisho wa kuonekana kwa Mungu, kwa kawaida huwa wazo la muda mfupi.
   2. Nyakati nyingine malaika wa BWANA; ilikuwa ni tendo la kuonekana kwake Mungu wakati mwingine ni mjumbe wa kimalaika wa Mungu.
   3. Melikizedeki pengine haikuwa tendo la kuonekana kwa Mungu, bali kilikuwa ni kivuli cha Kristo.
   4. Mtu wa nne katika moto pengine haikuwa ni tendo la kuonekana kwake Mungu, lakini malaika.
   5. Katika Agano Jipya, matendo ya kuonekana kwake Mungu katika Agano la Kale yalikuwa yanathibitishwa na kufanyika mwili (Yesu Kristo). Yesu ni zaidi ya dhihirisho (tendo la kuonekana kwake Mungu) Yeye ni Mungu katika mwili.

Maandiko ya kukariri: Yohana 1:18a; 4:24

Soma la 3
Majina na Vyeo vya Mungu

A. Maana kuu ya Majina ya Mungu
   1. Tabia (Kutoka 6:2, 7)
   2. Nguvu (Kutoka 9:16)
   3. Mamlaka (Kutoka 23:20-21)
   4. Uwepo/Kuwepo (1 Wafalme 8:27, 29, 43).

B. Majina na Vyeo vya Mungu katika Agano la Kale
   (Angalia orodha ukurasa 45-46.)
   1. Mungu
      a. Eli maana yake “nguvu, uwezo, mwenye nguvu zote, uungu.”
      b. Elohimu ni katika wingi, ukuu na uwezo, ni neno la kawaida la Kiebrania kumaanisha “Mungu”
   2. Bwana
      a. Adon linamaanisha “mtawala, Bwana.”
      b. Adonai ni aina ya mkazo; mara zote inamweleza Mungu.
   3. BWANA au Yehova
      a. YHWH (Yahweh) imetolewa katika msemo “kuwepo.”
      b. Linafanana na “MIMI NIKO” (Kutoka 3:14).
      c. Maelezo yake ni “Aliyeko wa Pekee, Aliye wa milele Pekee.”
      d. Ni jina la pekee ambalo Mungu alijitambulisha Mwenyewe katika Agano la Kale (Kutoka 6:3-8; Isaya 42:8).

C. Maendeleo ya Ufunuo wa Jina la Mungu
   1. Majina mchanganyiko ya Yehova. (Angalia orodha ukurasa wa 48-49.)
   2. Kutamani kulijua jina la Mungu.
   3. Ukamilifu katika jina la Yesu (Zekaria 14:9).

D. Jina la Yesu
   1. Lina maana Yehova Mwokozi au Yehova ni Wokovu.
      a. Inashirikisha kila kitu kinachodhihirishwa na Agano la Kale kuhusu Mungu (Yehova).
      b. Inadhihirisha kwamba Yehova amekuja katika mwili kuwa Mwokozi wetu (Mathayo 1:21, 23)
   2. Yesu Kristo wa Nazareti ndiye pekee anayefanania na kutimiza jina hilo. Jina Lake linadhihirisha:
      a. Tabia ya Mungu (mfano upendo) (Wakolosai 2:9)
      b. Nguvu za Mungu (mfano: miujiza) (Yohana 14:14; Matendo 3:6).
      c. Mamlaka ya Mungu (mfano; mafundisho) (Mathayo 28:18; Yohana 5:43).
      d. Uwepo kwa Mungu (ukamilifu wa roho) (Mathayo 18:20).
   3. Ni jina lililo juu zaidi (Matendo 4:10, 12; Waefeso 1:21; Wafilipi 2:9-11; Wakolosai 3:17).
   4. Siyo mfumo wa kiinimacho; lazima tuwe na imani katika Yesu Mwenyewe (Matendo 3:16; 10:43; 19:13-17).
   5. Kanisa la kwanza lilihubiri, lilifundisha, liliomba, lilitenda miujiza wagonjwa waliponywa, mapepo yalitolewa, walibatizwa, walioteseka, na kufurahia katika jina hilo.

Ukariri wa Maandiko: Matendo Matendo 4:12
Maelezo ya Elohim, Adonai, Yahweh.

Soma la 4
Yesu ni Mungu

A. Mafundisho ya Agano la Kale - Isaya 7:14; 9:6; 35:4-6 (na Luka 7:22); Mika 5:2.

B. Mafundisho ya Agano Jipya
   1. Lazima tutafsiri Agano Jipya katika mwanga wa msemo wa Agano la Kale na desturi.
      a. Wasomaji wa kale na waandishi walikuwa waaminio umoja wa Mungu.
      b. Waandishi walipomwita Yesu "Bwana" na "Mungu" walitumia maana ya Agano la Kale maana ya hayo maneno.
   2. Wakolosai 2:9 inafundisha uungu wa Yesu kikamili/kabisa.
      a. Ni mafundisho ya msingi (aya 8-10).
      b. Maneno matatu tofauti yanasisitiza ukweli huu: "utimilifu, wote, wa Uungu."
   3. Sehemu zingine zinazofundishaYesu ni Mungu aliyevaa mwili (Yohana 20:28-31; Matendo 20:28; Warumi 9:5; 2 Wakorintho 4:4; 5:19; Wakolosai 1:15, 19; Tito 2:13; Waebrania 1:3; 2 Petro 1:1; 1 Yohana 5:20).

C. Yesu ni Neno Lililofanyika Mwili (Yohana 1:1; 14)
   1. Maana ya ***neno*** katika Agano la Kale (Kiebrania, *dabhar):* Mungu anazungumza.
   2. Maana ya *neno* katika Agano Jipya (Kigiriki: *logos)*: neno lisiloelezeka (wazo, kusudi, mpango) au neno lililotamkwa (usemi, tendo)
   3. Neno ni akili ya Mungu, wazo, kusudi, mpango, ambao Mungu ni Mwenyewe. Neno alikuwa "pamoja" na Mungu katika hali ya linalomhusu" Mungu.
   4. Neno pia ni ufunuo wa Mungu Mwenyewe; Kujifunua binafsi kwa Mungu; Mungu kuwa wazi Mwenywe. Neno la milele, au Mungu Mwenyewe, alikuja katika mwili kama Mwana.

D. Kufanyika mwili kulitokea katika Mimba ya Kristo
   1. Yesu alikuwa ni Mungu katika uja uzito (Mika 5:2; Mathayo 1:23; Luka 1:35).
   2. Mtoto Yesu alipokea kuabudiwa/ibada kutoka kwa malaika, Simeoni, Anna, na mama jusi.
   3. Mungu alisababisha bikira kubeba mimba. Kwa hiyo Yesu alipokea hali ya uungu katika mimba, badala ya hali ya baba wa duniani.

E. Siri ya Utauwa
   1. Umoja wa Mungu hauna cha siri/fumbo kabisa; imeelezwa wazi kupitia Maandiko.
   2. Siri ya Utauwa ni kuu kwamba Mungu alidhihirishwa katika mwili (1 Timotheo 3:16) na imefunuliwa kwetu.

F. Yesu ni Baba aliyechukua Mwili
   1. Biblia ndivyo inavyofundisha (Isaya 9:6; 63:16; Yohana 10:30, 33, 38; 12:45; 14:6-11, 18; 1 Yohana 3:1-5; Ufunuo 21:6-7).
      a. Yesu alisema "Mimi na Baba tu umoja," badala ya Mimi ni Baba," kwa sababu Alikuwa vyote Baba na Mwana, vyote Roho isiyoonekana na mwili unaonekana.
      b. Yesu alisema "Mimi ni ndani ya Baba," kwa sababu kama vile mwanadamu mwingine yeyote, uanadamu Wake ulikuwa umetengana na kuunganika na Roho Iliyochukua mwili.
   2. Hali ya kimaandiko kuna matendo yasiyo ya kawaida kwa Baba na Yesu: kuufufua mwili wa Kristo, kupelekwa kwa mfariji, kuwavuta watu kwa Mungu, kuwafufua waliokufa kutoka katika wafu, kujibu maombi, kuwatakasa waamini.

G. Yesu ni Yehova aliyechukua Mwili
    1. Biblia inafundisha hivyo (Isaya 40:3, 5; Isaya 45:23 pamoja na Wafilipi 2:9-11; Isaya 52:6; Yeremia 23:5-6; Zekaria 11:12; 12:10; Malaki 3:1; Matendo 9:5; Ufunuo 22:6 na 16).
    2. Maandiko hutoa vyeo vingi vya namna ya pekee vya Yehova kwa Yesu, kama Mwenye nguvu, Mwamba, Pembe ya Wokovu, Mchungaji, Nuru, Mwokozi, Bwana, Mtakatifu Mmoja, Mwamuzi, wa Kwanza na Mwisho, Mfalme wa Israeli, Muumbaji, na Mkombozi angalia orodha ukurasa wa 68 na 69)
    3. Yesu ni Mimi Niko (Yohana 8:56-59; 10:38-39)

H. Yesu Ndiye Aliye kwenye Kiti cha Enzi
    1. Maelezo ya Aliye kwenye kiti cha enzi (Ufunuo 4:2, 8;) yanaligana na maelezo ya Yesu (Ufunuo 1:7-8, 11, 17-18).
    2. Yesu yuko “katikati ya kiti cha Enzi” au kiwazi “(amekaa) katikati ya kiti cha enzi” Ufunuo 5:6; 7:17).
    3. “Mungu na Mwana Kondoo” ndiye aliyeketi katika kiti cha enzi. Analo jina moja na uso mmoja (Ufunuo 22:3-4).
        a. Ni Yesu pekee Aliye Mungu na Mwana Kondoo, uungu na uanadamu, mtawala mkuu na dhabihu ya dhambi.
        b. Jina Yesu ni jina kuu zaidi (Wafilipi 2:9-11)
        c. Sura ya Yesu ni mfano unaoonekana wa Mungu asiyeonekana (Wakolosai 1:15; Waebrania 1:3).

Ukariri wa Maandiko: Isaya 9:6; Wakolosai 2:9-11; Yohana 1:11, 14; 10:30
Maelezo Neno (Logos)

Soma la 5
Mwana wa Mungu

A. Uungu na Uanadamu wa Yesu Kristo
   Lazima tuuthibitishe:
    1. Uhalisi na ukamilifu wa uungu wa Yesu.
        a. Tazama sehemu ya 4.
        b. Kutamka uungu Wake ni lazima (Yohana 8:24)
    2. Ukamilifu, uanadamu wa Yesu usiokuwa na dhambi.
        a. Uanadamu Wake kamili (Mathayo 26:38: Luka 2:40, 52; 22:42; 23:46; Matendo 2:31; Waebrania 2:14, 16-17; 5:7-8).
        b. Yeye hana dhambi (Waebrania 4:15; 1 Petro 2:22; 1 Yohana 3:5).
        c. Je! Yesu anaweza kutenda dhambi? Uanadamu Wake, autazamaye, alikuwa na hali sawa na Adamu, walakini kutokana na muunganiko wa uungu na uanadamu Asingeweza kutenda dhambi.
        d. Kukiri uanadamu Wake ni lazima (1 Yohana 4:3)
    3. Mtengano wazi wa uungu na uanadamu wa Yesu
        a. Angalia ordha ukurasa wa 83.
        b. Mfano namna tofauti katika ya (Warumi 5:8 na Wakolosai 1:27).
    4. Hali ya kutokutengana ya umoja wa uungu na uanadamu wa Yesu (Yohana 1:1, 14; 10:30, 38; 14:10-14; 16:32; 16:32; Waebrania 9:14).

B. Mafundisho mbali mbali ya Kristo Kihistoria
    1. Yesu alikuwa ni mwanadamu tu: (Ebonitism, Unitarianism)
    2. Yesu alikuwa ni roho tu: Docetism (katika Gnoticism)

3. Kristo alikuwa kiumbe cha kiungu ambaye kwa muda alikaa katika mwanadamu Yesu Cerintianism (katika Gnosticism)
4. Yesu alikuwa nafsi ya pili kiuungu mdogo kwa Baba: Subordinationism.
5. Yesu alikuwa ni mwanadamu ambaye kwa namna fulani alifanyika Mungu: Dynamic Monarchianism, Adoptionism.
6. Yesu alikuwa uungu ulioumbwa, au nusu mungu, lakini siyo Mungu mmoja wa kweli: Arianism.
7. Yesu alikuwa na hali kamili ya uanadamu: Apollinarianism.
8. Yesu alikuwa na asili moja, iliyomilikia na uungu: Monophysitism, Monothelitism.
9. Yesu alikuwa na asili mbili siyo katika kuwepo bali kwa ajili ya kusudi tu, kitendo, au kuonekana: Nestorianisim.
10. Mfumo wa kitamaduni (Council of Chalsedon 451): Yesu ni nafsi moja na hali mbili, uanadamu na uungu.
11. Tamati.
    a. Kwa mitazamo hii, pengine ya mwisho ni karibu sana na Maandiko ingawaje baraza na lugha yake walikuwa wana Utatatu.
    b. Nestrius pia alikuwa na vidokezo vya thamani/maana, kama vile kukataa kwake Mariamu kuitwa mama wa Mungu.
    c. Pengine ni bora zaidi matumizi ya maandiko manne kama uthibitisho wa kimaandiko katika A.
    d. Badala ya kuzungumzia zaidi “asili mbili” katika Kristo, pengine ni bora kuzungumzia hasa uanadamu na uungu Wake, au kuzungumzia Mungu mmoja aliyedhihirishwa katika Kristo na kwa wakati huo huo Kristo kama mwanadamu kamili.

C. Msemo Mwana wa Mungu
    1. “Kristo” inamaanisha Masihi, Mpakwa mafuta.
    2. Mwana.
        a. Mwana siyo nafsi ya kiungu bali ni umbo la mfano wa Mungu asiyeonekana (Wakolosai 1:13-15; Waebrania 1:1-3).
        b. Mwana alikuja kuwepo kwa bikira kuchukua mimba (Luka 1:35; Wagalatia 4:4)
        c. Maneno hayo yana elezea uanadamu wa Kristo (Warumi 5:10), au wakati mwingine umoja wa uanadamu na uungu (Mathayo 26:64; Waebrania 1:8-9).
        d. Kamwe hakuwahi kutumika kama uungu peke yake, wala haikuwahi kutumika mbali na uanadamu wa Kristo.
        e. Tamati: maneno yanaelezea Mungu kudhihirishwa katika mwili.
    3. “Mungu Mwana” katika tafsiri ya King James Bible katika Kiingereza na katika Kiswahili haimaanishi kuwa ni Mungu mwingine siyo matamshi ya ki-Biblia.
    4. Mwana wa Mungu
        a. Cheo huelezea Kristo kuwa amezaliwa na Mungu, na siyo baba wa kibinadamu.
        b. Pia inaelezea Kristo kuwa Mungu katika mwili. “Mwana wa” inamaanisha kuwa na tabia au hali ya.” Kama Mwana wa Mungu asiye wa kawaida, Yesu alizaliwa na hali halisi, au hali ya kufanana, na Mungu (Yohana 5:17-18; 10:33). Hii inamaana alikuwa Mungu, kwa maana hakuna mwingine anayeweza kuwa mkamilifu kama Mungu au kuwa sawa na Yeye. (Angalia Isaya 46:5, 9.)
    5. Mwana wa Adamu
        a. Cheo hiki kinamwelezea Kristo kama mwanadamu kamili au umbile halisi la kibinadamu.
        b. Pia ni hali ya Kimasihi
    6. Maneno *Neno* na *Mwana* yanahusiana lakini hayalingani.
        a. Neno ni Mungu wa milele lililodhihirishwa katika Mwana
        b. Mwana ni uanadamu; maneno haya yana kiwango katika Kufanyika mwili.

D. Mwana aliyezaliwa Dhidi ya “Mwana wa Milele”
    1. “Mwana wa Milele” siyo matamshi ya ki-Biblia.
    2. Mwanzo wa Mwana ilikuwa ni katika kufanyika mwili (Luka 1:35; Wagalatia 4:4 Waebrania 1:5).
    3. Mwisho wa utendaji wa Uwana kutatokea baada ya hukumu ya mwisho (1 Wakorintho 15:23-38; Waefeso 2:27).
        a. Hakutakuwako tena na hitaji la ukombozi au upatanishi.
        b. Uanadamu uliotukuzwa wa Yesu utakuweko milele (Ufunuo 22:3-4).

E. Makusudi ya Mwana.
    1. Kuleta ukombozi kwa wanadamu walioanguka katika dhambi, kama mwana kondoo wa dhabihu (kipatanishi), badili, jamaa ya karibu mkombozi, mpatanishi, msuluhishi, kuhani mkuu, wakili, Adamu wa pili, na mfano wa haki.
        a. Kuweka dhambi mbali
        b. Kuharibu kazi za shetani
        c. Kuliandaa Kanisa kwa ajili ya kuja Kwake mara ya pili.
    2. Kumdhihirisha Baba, kutumika kama mtume na nabii.
    3. Kuweka ufalme wa Kimasihi duniani.
    4. Kuhukumu ulimwengu.

F. Uumbaji kwa Mwana (Wakolosai 1:13-19; Waebrania 1:2)
    1. Yeye aliyekuja kufanyika Mwana aliuumba ulimwengu
    2. Mungu aliuumba ulimwengu na Mwana katika mtazamo wa (kutegemea Mwana, “kupitia” Mwana).
        a. Mungu alijua wanadamu watatenda dhambi.
        b. Mungu alijua kwamba ukombozi utakuwa kupitia Mwana, kwa hivyo kusudi Lake la awali litatimizwa kupitia Mwana (1 Petro 1:19-20; Ufunuo 13:8).
    3. Ingawaje Mungu hakuuchukua uanadamu hadi wakati mtimilifu ulipowadia, aliutendea kazi katika uumbaji.

G. Yesu kama Mzaliwa wa kwanza au Aliyetangulia kuzaliwa (Warumi 8:29; Wakolosai 1:18; Waebrania 1:6)
    1. Ndiye mwanadamu pekee aliyezaliwa na Mungu;
    2. Alikuwa wa kwanza katika mpango wa Mungu (angalia E-2.)
    3. Alikuwa ni wa mwanadamu wa kwanza kushinda dhambi.
    4. Alikuwa mwanadamu wa kwanza kushinda mauti/kifo
    5. Yeye ni mzaliwa wa kwanza (kama mzaliwa wa kwanza wa kiume) kichwa cha Kanisa, kichwa cha kiroho cha familia ya kiroho.

H. Tamati kuhusu Mwana wa Mungu
    1. Cheo Mwana wa Mungu mara zote inaelezea juu ya uanadamu wa Kristo, katika kufanyika mwili.
    2. Mara zote yanaelezea wakati/muda.
    3. Kama Mungu Yesu alikuwa na nguvu zote na kujua yote, lakini kama Mwana (uanadamu Wake), alikuwa na kiwango kujua.

Maandiko ya kukariri: Luka 1:35; Wagalatia 4:4
Maelezo: Mwana.

Soma la 6
Baba Mwana na Roho Mtakatifu

A. Baba
   1. Baba ni Mungu katika uhusiano wa uanadamu kiuzazi.
   2. Mungu ni Baba wa uumbaji wote (Kumbukumbu 32:6; Malaki 2:10; Waebrania 12:9)
   3. Ni Baba wa waamini waliozaliwa mara ya pili/waliookoka (Warumi 8:15)
   4. Ni Baba wa Mwana (Waebrania 1:5)
   5. Baba alidhihirishwa katika jina la Yesu (Yohana 5:43; 17:6, 26; Waebrania 1:4; 2:12)

B. Mwana
   1. Mwana ni Mungu katika mwili (angalia somo la V)
   2. Jina la Mwana ni Yesu (Mathayo 1:21);
   3. Hatusemi Baba ndani ya Mwana, lakini Baba yuko ndani ya Mwana (Yohana 14:10)

C. Roho Mtakatifu
   1. Roho Mtakatifu ni utendaji kiroho, hasa utendaji ambao ni Roho Mtakatifu pekee anaweza kutenda (Mwanzo 1:2; Matendo 1:4-5).
   2. Utakatifu ni hali ya maadili ya Mungu; Mungu ni “Aliye Mtakatifu”.
   3. Ukiroho ni asili ya Mungu isiyo ya kawaida “Mungu ni Roho”
   4. Ndiyo kusema kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe (Matendo 5:3-4; 1 Wakorintho 3:16; na 6:19).
   5. Roho Mtakatifu huja katika jina la Yesu (Yohana 14:26)

D. Baba ni Roho Mtakatifu
   1. Baba ndiye Mungu mmoja wa kweli (Yohana 17:3), na Mungu ni Roho Mtakatifu.
   2. Baba wa Yesu ni Roho Mtakatifu (Mathayo 1:18, 20; Luka 1:35)
   3. Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu, Yehova (Mwanzo 1:2; Isaya 40:13; Yoeli 2:27-29).
   4. Roho Mtakatifu ni Roho ya Baba (Mathayo 10:20)
   5. Kwa njia ya kipekee maandiko hutenda kwa pamoja kwa Baba na kwa Roho Mtakatifu, kumfufua Yesu, kufufua wafu, kuwapokea waamini, kukaa ndani ya waumini, kufariji, kutakasa, kutia nguvu, kutoa neno wakati wa mateso.

E. Uungu wa Yesu Ni Baba - (Angalia somo la IV-F)

F. Uungu wa Yesu ni Roho Mtakatifu
   1. Bwana ndiye Roho (2 Wakorintho 3:17)
   2. Roho Mtakatifu ni Roho wa Mwana, ambaye ni Yesu Kristo (Wagalatia 4:6; Wafilii 1:19)
   3. Roho Mtakatifu ni Kristo aliyefufuka (Yohana 14:16-18; 16:7). (Angalia pia Mathayo 18:20; 28:20; Wakolosai 1:27.)
   4. Hali ya maandiko inajieleza kipekee kwa pamoja kuhusu Yesu na Roho Mtakatifu: ikiendeleza unabii, kufufua waamini, kuufufua mwili wa Kristo, anakaa ndani ya waamini, kutakasa, kuwa wakili na mfariji, kuwa mwombezi, kutoa neno wakati wa mateso.

G. Marejeo ya Hali tatu
   1. Waefeso 3:14-17 inaweka wazi Roho Mtakatifu kama Roho wa Baba na pia kama Kristo
   2. Mathayo 28:19 inazungumzia jina moja linalofunua Mungu na hali/kazi yake kamili ya ukombozi, ambaye ni Yesu.
      a. Jina moja kuu ilikuwa lazima lifunuliwe (Isaya 52:6; Zekaria 14:9: Ufunuo 22:3-4).
      b. *Jina* katika Mathayo 28:19 ni umoja.
      c. Jina la Yesu linamdhihirisha Baba, Mwana, Roho Mtakatifu (Mathayo 1:21; Yohana 5:43; 14:26)

d. Mitume walitimiza agizo kwa kubatiza katika jina la Yesu (Matendo 2:38; 8:16; 10:48; 19:5; 1 Wakorintho 1:13).
e. Walitamka wazi jina la Yesu katika ubatizo (Matendo 22:16; Yakobo 2:7). (Angalia pia Matendo 3:6; 4:10.)
f. Jina la Yesu lilikuwa na linajulikana pia katika maagizo mengine katika kazi ya Injili (Marko 16:17; Luka 24:47).
g. Jina la Yesu ndilo jina pekee lililotolewa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na hivyo ni lazima litumike katika ubatizo, ambao ni kwa ajaili ya ondoleo la dhambi (Matendo 2:38; 4:12; 10:43).
h. Katika fungu la maneno la Mathayo 28:19, Yesu ndiye picha ya msingi. Kwa sababu alikuwa na mamlaka yote, aliwaagiza wafuasi Wake kuwafanya watu wanafunzi kwa ajili Yake na kuwabatiza kwa jina Lake.

3. 1 Yohana 5:7.
   a. Aya hii inaelezea aina tatu za mafunuo ya kimbinguni: Baba, Neno na Roho.
   b. Maneno ya kibinadamu na roho yake siyo vitu viwili tofauti naye, ila ndizo njia tofauti anazofahamika nazo.
   c. "Watatu hawa ni Umoja" inazungumzia utambulisho, siyo zaidi umoja au makubaliano (tofautisha na aya ya 8.)
   d. Wasomi wa utatu kwa kawaida husema kwamba aya hii haikuwa sehemu ya Maandiko ya awali.

H. Tamati
1. Kazi hizo tatu ilikuwa ni lazima kwa ajili ya mpango wa wokovu.
   a. Mwana: Mwanadamu asiyekuwa na dhambi ilikuwa ni lazima kwa ajili ya dhambi
   b. Baba: Uzazi wa Baba na mahusiano na Mwana
   c. Roho Mtakatifu: Mungu akifanya kazi katika maisha ya mwanadamu kufanya upya, kutakasa, na kutia nguvu.
2. Maneno Baba, Mwana, Roho Mtakatifu inaelezea ufunuo wa kazi ya Mungu ukombozi, kazi maadhihirisho, aina ya utendaji, vyeo, utendaji, ofisi, au mahusiano ya Mungu mmoja na wanadamu.
3. Mungu haelezewi kwa, au kuwa na kiwango, umuhimu wa utatu; Yeye ni mmoja halisi. Kwa mfano: Mtu mmoja anaweza kuwa na hali tatu zitendazo kazi au mahusiano – kama vile utawala, mwalimu, mshauri – na bado akawa ni mtu mmoja katika kila hali.
4. Mungu si nafsi tatu, na wala hakuna Mungu watatu. Mungu hana asili mbili za dhamiri, hali binafsi, mapenzi, nia, wala mwili.

Maandiko ya kukariri: Mathayo 28:19; 2 Wakorintho 3:17
Maelezo: Baba Mwana na Roho Mtakatifu.

Soma la 7
Maelezo ya Agano la Kale

A. Mfumo wa Wingi wa Elohim
1. Mfumo wa wingi unawakilisha ukuu, umakini, au ukuu katika Kiebrania, na imetumiwa sana katika uhusiano na Mungu mmoja. Mifano: dhihirisho moja kwa Yakobo; Yesu (Mwanzo 32:30; Zaburi 45:6; Zekaria 12:8-10; 14:5).
2. Hata katika sehemu zingine za maandiko, hili neno mara kwa mara linaelezea kuwepo mmoja. Mifano ndama wa dhahabu, mmoja wa miungu ya wapagani (Kutoka 32:4; Waamuzi 8:33; 11:24).

B. “Na Tumfanye Mtu” (Mwanzo 1:26)
    1. Muumbaji hakika ni mmoja (Mwanzo 1:27; Isaya 37:16; 44:24)
    2. Mfano wa kiumbe, mwanadamu, ni mtu mmoja katika uhalisi wake, na kwa njia hii inamfananisha na mfano wa Muumbaji.
    3. Uwezekano wa matamshi ya wingi
        a. Mungu alijishauri na mapenzi yake Mwenyewe (Waefeso 1:11).
        b. Ni ukuu au wingi wa kawaida (Danieli 2:36; Ezra 4:18; 7:23-24).
        c. Mungu aliwaarifu malaika mpango Wake (1 Wafalme 22:19-22; Ayubu 38:4-7).
        d. Inakubaliana na mfumo wa wingi wa Elohim.
        e. Ni maelezo ya kiunabii kwa Mwana. (Angalia somo la V-E.)

C. Matamshi Mengine ya Wingi (Mwanzao 3:22; 11:17; Isaya 6:8)
    1. Mungu alikuwa anawasemesha malaika.
    2. Isaya 6:8 inaweza kuwa inazungumzia wenye haki.

D. “Moja” (Echad) katika Kumbukumbu 6:4
    1. Je! Hii inamaanisha wingi katika umoja au umoja?
    2. Fungu hili la maandiko linazungumzia wingi katika umoja kihesabu, kwa vile sehemu hiyo inapinga umoja katika wingi. Kama inamaanisha tu umoja, basi inapinga ushirika wa nafsi lililotengana na halipingi wingi katika umoja.
    3. Echad lina maana moja kihesabu/kiidadi katika sehemu nyingi kimaandiko. Mifano: Joshua 12:9-24; Ezekieli 33:24.

E. Madhihirisho ya Mungu (Theophanies)
    1. Madhihirisho yote yanaweza kuelezwa kwa kuwepo kwa mmoja mwenye nguvu zote, Mungu mwenye kuenea pote.
    2. Aliyekuwa “mtu” wa ziada aliyemtokea Ibrahimu walikuwa ni malaika.
    3. Malaika wa BWANA wakati mwingine anaweza kuwa dhihirisho la Mungu; katika nyakati nyingine ni malaika hutofautisha kutoka Mungu lakini atendaye kama mjumbe wa Mungu au wakala.

F. Marejeo kuhusu Mwana na Masihi. Yote ni unabii.

G. Neno la Mungu
Neno la Mungu ni maelezo Yake, siyo nafsi tofauti mbali Naye (Zaburi 107:20; Isaya 55:11).

H. Hekima ya Mungu
    1. Hekima ni tabia yaMungu, siyo nafsi tofauti Kwake.
    2. Mithali huelezea hekima hutoa sauti (Mithali 1:20).

I. Marudio ya aina Tatu
    1. “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu” (Isaya 6:3) imetumiwa kusisitizia, kama ilivyo katika Yeremia 22:29.
    2. Marudio ya “Mungu” na “BWANA” kiurahisi yametumiwa tu kuelezea sehamu ya matumizi ya kawaida. Mifano: mibaraka mitatu kwa pamoja; Mungu akijisemea Mwenyewe katika hali ya tatu; tumia majina mawili kwa pamoja “BWANA MUNGU.” (Kwa mfano Mwanzo 2:7.)

J. Roho wa Mungu
    1. Roho ni hali ya Mungu kiroho, utendaji wa kiroho, na kutenda kazi kati ya wanadamu.
    2. Roho siyo nafsi pekee, kama vile mwanadamu na roho yake isivyo nafsi tofauti.

K. Mzee wa siku na Mwana wa Adamu (Danieli 7:9-28)
    1. Mzee wa Siku ni Yesu (Ufunuo 1:12-18)
    2. “Mmoja kama Mwana wa Adamu “ ni mfano wa watakatifu (Danieli 7:13, 18, 22, 26-27)
    3. Kama “mmoja kama Mwanadamu” ni Yesu, basi hilo linafananisha na utendaji wake katika uanadamu.

L. Mwenzake na Yehova (Zekaria 13:7)
Masihi siyo mwenzi wake Mungu, bali ni mtu mwenye ushirikiano kamili na Mungu.

Soma la 8
Maelezo ya Agano Jipya: Injili

A. Misaada Minne Muhimu katika Kufahamu
    1. Maelezo ya wingi humwelezea Yesu katika uanadamu na Uungu wa Yesu.
    2. Wakati mwingine Yesu alinena na kutenda akiwa kazini kama Mungu au kumwelezea akiwa mwanadamu katika hali zote mbili.
    3. Maelezo mengine ya wingi wanakuwa hivyo kutokana na majukumu yake uhusiano wake na binadamu, madhihirisho, na aina mbalmbali za utendaji, na mwelekeo wa ufunuo wa Mungu mwenyewe.
    4. Waandishi wa Agano Jipya na wasomaji hawakuwa na wazo la utatu, kwa kuwa wazo hilo na maneno kwa maelezo yalikuwa hayajawekwa. Baadhi ya sehemu za maadishi zinaweza kuwa ngumu kutokana na tafsiri za wa-utatu kwa karne nyingi.

B. Ubatizo wa Kristo
    1. Sauti na njiwa hazihitaji nafsi tofauti; mmoja mwenye nguvu zote; Mungu anaenea pote anaweza kujidhihirisha kwa njia/hali isiyo dhahiri kwa namna/njia mbali mbali.
    2. Wale waamini wenye msimamo wanaofuatilia Umoja wa Mungu hawakuelezea kwamba walipokea mafunuo mapya ya wingi katika Mungu.
    3. Njiwa alikuwa ni mfano wa kupakwa mafuta na ishara kwa Yohana Mbatizaji (Yohana 1:32-34)
    4. Sauti ilikuwa ishara kwa ajili ya watu (Yohana 12:28-30).
    5. Makusudi yalikuwa ni kwa Yesu kupakwa mafuta kimamlaka kama Masihi, kwa ajili ya mwanzo wa huduma Yake.
    6. Sauti ya kimbinguni katika matukio mengine mawili yanaweza kuwa hivyo hivyo kuelezea kama ishara ya kimiujiza.

C. Maombi ya Kristo
    1. Yalikuwa ni maombi kutoka katika hali halisi ya maisha ya binadamu. Kwa kuwa Yesu alikuwa Mungu kweli na kuweka mfano kwa ajili yetu, Aliomba.
    2. Maombi yanaendana na uanadamu tu, kwa kuwa Mungu hahitaji kuomba.
    3. Kama Yesu aliomba kama nafsi ya pili, basi hakuwa Mungu kweli bali alikuwa chini/ msaidizi kwa nafsi ya kwanza, ikipingana na mafundisho ya kiutatu kuwa wako sawa.
    4. Hatusemi kwamba Yesu alijiomba Mwenyewe; msemo huo hauko sahihi kwa sababu itakuwa kwamba alikuwa na hali ya uanadamu tu, kama sisi. Badala yake, kama mwanadamu tu, Yesu aliomba kwa Mungu, na kwa wakati huo huo Mungu alikuwa kweli kajidhihirisha ndani Yake.

D. “Mungu wangu Mungu wangu Mbona Umeniacha?” (Matahayo 27:46)
    1. Roho wa Mungu hakuandoka hasa katika mwili wa Yesu hadi kifo Chake (Yohana 10:30; 16:32).

2. Yesu alidhihirisha hisia za uanadamu halisi Alipopata hali ya kuachwa na Mungu – mtengano ambao wenye dhambi ambao hawajatubu watakayoipitia katika hukumu ya mwisho.
3. Roho wa Mungu bado alikuwa ndani ya Kristo lakini hakuukinga uanadamu Wake kutoka katika maumivu ya mateso halisi ya kibinadamu.
4. Yesu alinukuu maneno ya Daudi katika Zaburi 22:1. Daudi siye aliyekuwa ameachwa hasa, lakini alijisikia kuachwa.

E. Mawasiliano ya Maarifa kati ya (Watu) Nafsi Katika Uungu?
   1. Mabishano haya yanaelekeza kwenye hali tatu tofauti katika Uungu, ambao ni utatu.
   2. Mawasiliano ya maarifa kati ya nafsi za kiungu?
      a. Mathayo 11:27: Hakuna yeyote anayeweza kuelewa hali ya kufanyika mwili isipokuwa kwa ufunuo wa mbinguni, na njia pekee ya kumfahamu Mungu katika utimilifu Wake ni kupitia Yesu Kristo.
      b. Yohana 16:13: Waamini waliojazwa Roho hawana mamlaka pekee; Roho ndani yao atasema tu kile kinachoendana na nia na mapenzi ya Mungu.
      c. Warumi 8:26-27: Mungu anaye hamasisha maombi yetu na kutusaidia kuomba pia husikia maombi yetu na hujibu maombi yetu. Hutenda kazi katika usawa Mwenyewe huyajibu maombi yale yaliyo katika mapenzi Yake mwenyewe.
      d. Katika 1 Wakorintho 2:10-11: Mungu huyafunua mambo kwetu kupitia Roho Wake katika maisha yetu, Huitwaa kweli kutoka katika akili Yake na kuiweka kwetu. Lakini Mungu na Roho Wake siyo nafsi mbili zaidi ya mwanadamu na roho yake vilivyo.
      e. Tamati: Aya hizi zinaelezea umaana (siyo umuhimu) tofauti kati ya Mungu kama Aonekanavyo katika ukuu Wake, uwezo Wake na kuenea Kwake pote na hali ya kutwaa mwili au Mungu kama Atendavyo kazi katika mioyo ya wanadamu.
   3. Upendo kati ya nafsi za Mungu?
      a. Mungu ni pendo, jambo hilo halihitaji wingi, nafsi za milele. Kwa mfano, Alitupenda kabla ya uumbaji.
      b. Pendo kati ya Baba na Mwana (Yohana 3:35; 14:31; 17:24). Mungu alimpenda Mwanadamu Kristo Yesu kama anavyowapenda wanadamu wote, na mwanadamu Kristo alimpenda Mungu kama watakiwavyo wanadamu wote.
      c. Kabisa Roho Mtakatifu hajatajwa kama sehemu itakiwayo katika mahusiano ya pendo.
   4. Imani/Ungamo kati ya nafsi za Mungu?
      a. Baadhi huwa wana toa mifano ya kiunabii mbalimbali kuhusiana na kufanyika mwili kujako. Mifano Zaburi 40:6-8; Waebrania 10:5-9.
      b. Wengine huelezea kwamba Yesu ni mwanadamu halisi akimwomba Mungu.
      c. Sauti kutoka mbinguni ilikuwa ni ishara kwa watu (Yohana 12:30).
      d. Roho Mtakatifu kabisa hakuwa sehemu ya haya mazungumzo.

F. Kutangulia kuweko kwa Yesu
   1. Kama Mungu (Roho, Yehova) Yesu alitangulia kuwepo katika maisha Yake ya ulimwenguni, lakini siyo kama wanadamu (mwana) (Yohana 5:58).
   2. Kabla ya kufanyika mwili, Mwana alikuweko tu katika mawazo ya Mungu kama mpango aliotangulia kuupanga (Yohana 17:5; 1 Petro 1:19-20). (Angalia somo la V-D.)
      a. Utukufu aliokuwa nao na Baba kabla ya uumbaji na kuomba kupokea unaohusiana na kusulubishwa na ufufuo Wake.
      b. Alizungumzia juu ya kuwapa wanafunzi utukufu huu (Yohana 17:22), lakini Mungu hashiriki katika utukufu wa kiungu.
      c. Mara zote Yesu ana utukufu Wake kama Mungu na hakuhitaji yeyote kuurudisha Kwake.

3. Yesu Kristo “Alitoka kwa Baba” (Yohana 16:28).
    a. Asili yake ni uungu, siyo uanadamu: Alizaliwa na Mungu, siyo mwanadamu, katika tumbo la bikira.
    b. Uungu katika uungu wa Kristo katika uanadamu ni Baba: Baba Alijiunganisha Mwenyewe na uanadamu kumleta Kristo kuwepo.
4. Yesu alitoka mbinguni (Yohana 6:38, 62)
    a. Aya hizi zinaelezea kufanyika mwili: Mungu alikuja duniani kama mwanadamu (kama Yesu, Mwana).
    b. “Mwanadamu” katika Yohana 6:62 ni sawa na “Mimi.”

G. Mwana Alitumwa toka kwa Baba
1. Neno aliyetumwa katika Yohana 3:17; 5:30 haelezei kutangulia kuweko kwa Mwana.
    a. Yohana mbatizaji “aliyetumwa” yeye hakuwepo tangu mwanzo (Yohana 1:6)
    b. Mwana “alitumwa kwa kuzaliwa na mwanamke (Wagalatia 4:4).
2. Neno lilitumwa kutimiza kusudi. Mwana alizaliwa na kuwekwa kwa ajili ya kazi maalumu.

H. Sifa zingine katika ya Baba na Mwana
1. Aya nyingi zinazungumzia utofauti kati ya Baba na Mwana katika nguvu, na ukuu na maarifa (Marko 13:32; Yohana 5:19; 6:38; 14:28)).
2. Kama yangeonyesha nafsi mbili za uungu, basi Mwana si Mungu halisi au mdogo kuliko Baba, ikipingana na fundisho la utatu la kuwa wote ni sawa.
3. Hakika, aya hizi zinahusiana na uanadamu wa Yesu. Katika uanadamu Wake, au hali Yake ya Uwana, alikuwa na kiwango; lakini kwa hali yake ya kiungu Hakuwa na kikomo.
4. Mungu Hakupoteza nguvu Zake, kuenea kwake kote, au uwezo wa kujua yote kuenea Kwake kote katika kufanyika mwili. Wakati Mungu alipofunuliwa kikamilifu katika Kristo, Roho wa Kristo – Baba – bado Alikuwa anaenea pote.
    a. Yesu alikuwa mbinguni na duniani wakati huo huo (Yohana 3:13).
    b. Bado Mungu anawasiliana na kudhihirisha uwepo Wake (“uso”) kwa njia ile ile kwa malaika mbinguni (Mathayo 18:10).

I. Matumizi Mengine ya Wingi
1. Vifungu vya “Na” (Yohana 1:1-2; 1 Yohana 1:2)
    a. Maana yake ni kufungamana na, mali ya, ndani ya.”
    b. Maelezo binafsi ya Mungu, mpango wa Mungu wa kutwaa mwili, na uzima wa milele vilikuwa “ pamoja na” Mungu katika ufahamu uliokuwa Naye na kuwa Yeye halisi, siyo nafsi tofati.
2. Mashahidi wawili (Yohana 8:16-18).
    a. Roho wa Mungu na mwanadamu Kristo vyote hushudia kwamba Yesu alikuwa Mungu katika mwili.
    b. Mifano: Kwa maajabu Mungu alisema kutoka mbinguni; kama mwanadamu Kristo alishuhudiwa maneno na vitendo vya kibinadamu.
3. Matumizi ya Wingi ya Baba na Mwana, “wote, nao, sisi, siyo pekee, pamoja” (Yohana 8:19, 29; 15:23-24; 16:32; 1 Yohana 2:23; 2 Yohana 9).
    a. Yesu hakuwa mwanadamu tu, bali Alikuwa Mungu pia.
    b. Yesu hakuwa peke Yake, Alikuwa na Roho wa Mungu ndani Yake.
    c. Yesu alikuwa ni zaidi ya Baba anayeonekana. Alikuwa vyote Baba na Mwana, Roho na Mwili.
    d. Kwa vile Yesu ni Baba aliyeutwaa mwili, tunapoona, kujua, kuamini, na kumkiri Yeye siyo kwamba tunaona tu, kujua, kuamini, na kimkiriri Mwana bali pia Baba.
4. Ushirika na Baba pia na Mwana (Yohana 14:23; 17:21-22).

a. Fungu hilo linazungumzia ushirika, siyo kihalisi kuingia kwa roho mbili za kiungu.
b. Tumeunganishwa na Mungu kupitia mwanadamu Kristo na upatanisho Wake.
c. Tuna ushirika na Mungu kama mwanadamu Kristo alivyokuwa.
d. Sifa za hali zote mbili. – Baba – na Mwana – wako kwetu. Mfano: nguvu ya Mungu; utii, unyenyekevu na kujishusha kwa Yesu.
e. Njia ambayo tumeunganika nayo sana ni Roho mmoja kuwa ndani yetu (siyo tatu) - Roho Mtakatifu, au Roho wa Kristo.
f. Tuna ushirikiano mmoja na Roho mmoja, nafsi moja, hatuwezi kujitambulisha kwa mahusiano matatu au nafsi tatu tofauti.

J. "Mfariji Mwingine" (Yohana 14:16-18)
1. Mfariji siyo nafsi nyingine, lakini ni ambaye wanafunzi tayari walikuwa wamekwisha kumjua ambaye tayari alikuwa "pamoja" nao.
2. Tofauti itakuwa ni mfumo mmoja au mahusiano tu. Muda si mrefu Mfariji atakuwa "ndani" yao.
3. Kwa maneno mengine, Yesu atarudi katika Roho. (Angalia Mathayo 28:20; Yohana 16:17; Waefeso 3:16-17.)
4. Kwa maneno mengine Mfariji "mwingine" ni Kristo katika Roho badala ya mwili, akikaa ndani ya waamini badala ya kuwa pamoja nao kimwili.

K. Umoja wa Kristo na Baba
1. Katika uanadamu Wake, Yesu alikuwa na Baba katika dhana ya kusudi moja, nia, na mapenzi (Yohana 17:21-22).
2. Katika hali hii Wakristo wanaweza kuwa mmoja na Mungu na kila mmoja.
3. Lakini pia Yesu ni mmoja na Baba katika hali ya uungu na utambulisho (Yohana 10:30-33; 14:9). Wakristo hawako mmoja na Mungu katika dhana na hali hii.

Soma la 9
Maelezo ya Agano Jipya: Matendo hadi Ufunuo

A. Mkono wa Kuume wa Mungu
1. Kwa vile Mungu ni Roho isiyoonekana, hana mkono wa kuume wa kimwili mbali na kufanyika mwili.
2. Fungu hilo la maneno/msemo huo ni mfano au umbile fananishi. Mifano (Zaburi 16:8; 77:10; 98:1; 109:31; Isaya 48:13; Luka 11:20).
3. Inaelezea nguvu, mamlaka, madaraka, mshindi pekee, ushindi, kuinuliwa, na wokovu. Mifano: (Kutoka 15:6; Zaburi 98:1; 110:1; Mathayo 26:64; Waefeso 1:20-22; 1 Petro 3:22).
4. Kristo aliyeonekana ameinuliwa na kuwa na nguvu zote, mamlaka, na madaraka ya Mungu asiyeonekana.
5. Aya pia inazungumzia Krsito aliyepo ambaye ni kazi Yake kama mpatanishi (Warumi 8:34; Waebrana 8:1).
6. "Maneno amekaa chini" inaashiria mwisho wa kazi ya upatanishi wa Kristo (Marko 16:19; Waebrania 1:3; 10:11-13).
7. Stefano hakuwa na nafsi mbili za uungu; aliona Kristo aliyeinuliwa akiwa na utukufu wote wa Mungu, na kumwita Kristo pekee.

B. Salaam katika nyaraka (Warumi 1:7; 1 Wakorintho 1:3).
1. Salaamu hazifundishi utatu. Kama zinafundisha
   a. Kwa nini Roho Mtakatifu hakuwahi kutajwa?
   b. Baadhi ya vifungu vya maandiko vingefundisha nafsi nne (Wakolosai 2:2; 3:7).

2. Yanasisitizia hitaji la kumpokea Mungu katika maeneo mawili. Wokovu wetu una msingi juu ya utambulisho wa Mungu kama Baba na Muumbaji, lakini pia kutwaa kwake mwili kama Kristo.
3. Neno la Kigiriki "na" (*kai)* haihitaji nafsi mbili. (Angalia jedwali uk. 214-215).
    a. Wakati mwingine *kai* ina maanisha "hata" au "Aliyoko" (2 Wakorintho 1:2).
    b. Sheria ya Granviille Sharp inaendana na baadhi ya matukio: Kama majina mawili ni namba moja, jinsia, na jambo ambalo lina mahusiano na *kai* na kama majina ya awali yana kanuni halisi lakini ya pili haina, basi yale ya awali yana maana ya kitu hicho hicho. Mifano Wakolosai 2:2; 2 Wathesalonike 1:12; Tito 2:13; 2 Petro 1:1.
4. Maneno "Mungu na Bwana wa Bwana wetu Yesu Kristo" inaonyesha agano letu jipya la mahusiano na Mungu kupitia Kristo, sawa na na msemo "Mungu wa Ibrahimu" chini ya Agano la Kale.

C. Mbaraka wa Mitume (2 Wakorintho 12:14)
1. Aya hii inazungumzia karama tatu za kazi ya Mungu. Kutumia majina au vyeo vya Mungu mengi yake yanahusiana kwa ukaribu na kila moja.
2. Pendo ni hali ya milele ya Mungu
3. Neema hasa huja kupitia Upatanisho.
4. Ushirika wetu na Mungu na watakatifu wengine ni kwa Roho Mtakatifu.
5. Wana utatu wanakiuka mafundisho yao wenyewe kwa kudhania kwamba "Mungu" inaelezea kwa mmoja tu au kati ya nafsi tatu za kiungu (Baba). Je! nafsi hii kwa namna fulani ni Mungu zaidi kuliko wengine wawili?

.

D. Ushahidi wa Aina Tatu Nyingine
1. Waefeso 4:4-6: Mungu mmoja ni Roho na Bwana wa yote.
    a. Imani yetu na ubatizo hasa vina msingi katika kazi ya upatanisho ya Bwana Yesu.
    b. Roho mmoja wa Mungu hutubatiza katika mwili na kukaa ndani yetu.
2. Waebrania 9:14: Kwa nguvu ya Roho Wake akaaye ndani, Yesu aliutoa uhai Wake wa uanadamu kama dhabihu ili kutosheleza lile linalohitajiwa na sheria ya Mungu.
3. 1 Petro 1:2: Kutangulia kujua ni sehemu ya tabia/hali ya Mungu kabla ya kuutwaa mwili; damu ilikuwa imemwagika kama matokeo ya kuutwaa mwili; na utakaso ni kazi ya kiroho ya Mungu.
4. 1 Petro 3:18: Kristo alikufa kama mwanadamu, lakini alifufuliwa kwa nguvu iliyokuwa ndani Yake ili kumpatanisha mwanadamu na Mungu.
5. Yuda 20-21: Pendo ni sehemu ya hali asili yaMungu ya milele; rehema huja kupitia Upatanisho; na maombi ni kazi ya Kiroho.

E. Ukamilifu wa Mungu
1. Yesu ni Mungu aliyeutwaa mwili; katika Yeye hukaa utimilifu wote wa Mungu kimwili (Wakolosai 2:9).
2. Jifunze fungu la maneno ambayo Wakolosai kwa msisitizo yanathibitisha uungu wa Yesu Kristo. (Angalia jedwali ukurasa wa 225.)
3. Tunaweza kuwa na ukamilifu wa Mungu ndani yetu kwa kupokea Roho wa Kristo (Waefeso 3:19).
4. Sisi hatujifanyi miungu, lakini tunayo hali ya ukamilifu wa Mungu kupitiaYesu Kristo. Yesu pekee ndiye Ukamilifu pekee wa Mungu kwa utambulisho.

F. Kujinyenyekeza kwa Yesu (Wafilipi 2:6-8)
1. "Alikuwa yu na namna ya Mungu" ikimaanisha "kuwa Mungu halisi" Yesu alikuwa ni Mungu mmoja wa kweli aliyeutwaa mwili).

2. Hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kiti cha kushikamana nacho" maana yake hakuona kule kuwa Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho"
    a. Roho wa Kristo alikuwa ni Mungu halisi
    b. Yesu Kristo, Mungu aliyeutwaa mwili, alikuwa sawa na Mungu katika hali yake ya uungu. Nafsi ya mwanadamu wa kiungu alikuwa sawa na Mungu katika nguvu, mamlaka kwa kisichodhihirika, Roho ambayo haijafunuliwa.
    c. Walakini, Yesu hakusisitiza juu ya utauwa wa haki pekee ya utukufu uonekanao, heshima, ukuu, kuinuliwa.
3. "Alijifanya mwenyewe kuwa si kitu" maana yake alijishusha". Katika maisha Yake na huduma Yesu alikuwa mnyenyekevu na hiari ya kujinyenyekeza katika hali ya kibinadamu, kujishusha, na mauti.
4. Yesu hakuacha tabia zake za kiungu, kinyume na kile wana utatu wengi wanacho fundisha.
    a. Mungu hawezi kujitenga mwenyewe na Tabia Zake au hali.
    b. Yesu asingekuwa Mungu, mungu mdogo kama ilivyo katika mafundisho ya Ariani (Arianisim).

G. Mwana Kondoo katika Ufunuo 5
1. Maono ya Mwana Kondoo ni mfano; hatutaona kondoo halisi mbinguni, aliyechinjwa, akiwa na macho saba na pembe.
2. Mwana Kondoo anawakilisha upatanisho – Yesu katika uanadamu Wake, kazi ya dhabihu.
3. Mwana Kondoo inahusiana na uanadamu wa Kristo tu, kwa kuwa uanadamu tu hufa, siyo uungu.
4. Mwana Kondoo hasa ametoka katika kiti cha enzi, ikiwakilisha kutwaa mwili (Ufunuo 5:6; 7:17; 22:3-4).
5. Moja juu ya kiti cha enzi inawakilisha Uungu, ambao Yesu anao.
6. Yesu ndiye aliye katika kiti cha enzi. (Anagalia IV-H.)
7. Ufunuo 3:5 inaonyesha picha ya upatanisho wa Kristo.
    a. Tunatangaza haki katika uwepo wa Mungu kwa upatanisho wa Kristo.
    b. Katika hukumu tutasimama mbele ya mmoja – Yesu – siyo wawili (Yohana 5:22; 2 Wakorintho 5:10; Ufunuo 20:11).
8. Ufunuo 3:21 inaelezea kuwa tutatawala pamoja na Yesu katika ufalme Wake wa Kimasihi.
    a. Tutatawala pamoja naye kama wafalme na makuhani (Ufunuo 1:6), lakini hatamshirikisha mwingine utukufu Wake.
    b. Kuna kiti kimoja tu cha enzi cha uungu, kikiwakilisha ukuu, na Yesu pekee ndiye aketiye hapo. (Angalia IV-H.)

H. Kwa nini Mungu ameruhusu Aya zinazochanganya?"
1. Zinaeleweka zinapokuwa zimejifunzwa kutoka katika msingi wake na vifungu, ambavyo siyo vya utatu.
2. Mungu ametumia matamshi magumu kuwashinda wale wasio na njaa na kutafuta ukweli lakini wanatoshelezwa na mapokeo ya kibinadamu (Mathayo 13:13-15; Yohana 6:41, 51-60, 66).

I. Tamati
1. Yale yanayosemekana ni uthibitisho wa ki-utatu yanaweza kuelezewa katika njia ambayo si ya kiutatu kuoanisha na sehemu za maandiko iliyosalia.
2. Baadhi ni maandiko yenye nguvu ya Umoja wa Mungu.

3. Wa-utatu hutumia vifungo hivyo vinavyo waelekezea kwenye mapotofu zaidi, kama vile Arianisim, Subordinationisim, Binitarianisim (mafundisho ya nafsi mbili), trithesim (Utatu).

Soma la 10
Waaminio Umoja wa Mungu katika Historia ya Kanisa

A. Kutazama kwa ujumla
   1. Mafundisho ya umoja wa Mungu yanmsingi katika maandiko, siyo historia, mapokeo wala ukiri.
   2. Tunaweza kuchora/kuandika maana/hoja tatu za kihistoria.
      a. Mababa-wa kimitume wa kanisa la kwanza walikuwa waaminio wa Umoja wa Mungu, kabisa hawakuamini utatu.
      b. Utatu ulijitokeza baadaye katika wakati wa karne ya pili lakini haikuwa imani iliyoenea hadi kama mwaka wa 300 baada ya Kristo na haikuwa imeanzishwa kiulimwengu hadi kama mwaka wa 400.
      c. Uimani ya Mungu mmoja iliendelea kuwepo moja kwa moja katika historia.
   3. Taarifa za kihistoria zinazohusu umoja wa Mungu ni chache na pengine zimeharibiwa.
      a. Historia ilikuwa imeandikwa na wapinzani wa Umoja wa Mungu.
      b. Katika hali zote "wanafiki" hawakuacha kumbukumbu zozote zilizoandikwa, au maandishi yaliharibiwa.
   4. Hatuelewi kiulazima juu ya mafundisho ya watu wafuatao, lakini inaonekana walikuwa na msimamo na itikadi muhimu ya mtazamo wa Umoja wa Mungu.

B. Wanaoamini Umoja wa Mungu kuanzia Karne ya nne Hadi leo. (Karne ya Pili B. K)
   1. Viongozi wa awali wa kimitume na waandishi walikuwa ni Clement, Polycarp, Ignatus na Hermans (90-140 BK.)
      a. Walithibitisha Umoja wa Mungu katika Agano la Kale na uungu na uanadamu wa Yesu Kristo. Ignatus kwa kurudia rudia alielezea kuwa Yesu Kristo "Mungu wetu"
      b. Hawakutumia matamshi ya utatu wala mawazo, lakini walishikilia kwa ukaribu msemo wa lugha ya Biblia.
      c. Baadhi walifanya marejeo kwa ubatizo katika jina la Yesu.
      d. Inaoneka kwamba walikuwa waamni wa muhimu sana wa Umoja wa Mungu.
   2. Irenaus (alikufa mwaka 200 B.K. alikuwa ni mwana theolojia maarufu sana.
      a. Kwa nguvu sana alisisitiza kwamba Yesu alikuwa Mungu aliyeuvaa mwili na kusema Logos alikuwa ni wazo la Mungu na dhihirisho linaloonekana la Baba.
      b. Pengine aliamini katika uchumi wa utatu au utatu wa madhirisho.
   3. Baadhi ya maelezo ya nyakati za kati na karne ya pili yanaelezea hisia ya mfumo wa imani ya utatu. Kwa mfano: *Didache* anazungumzia kuhusu mifumo mitatu ya ubatizo (lakini pia ubatizo katika jina la Bwana)
      a. Wasomaji wa utatu wanaweza kuelewa vibaya baadhi ya maelezo haya, kama vile wafanyavyo Biblia.
      b. Kuna uwezekano mkubwa wa kuongeza maneno (nyongeza) yaliyofanywa na nakala za wana utatu waliofuata.
      c. Mafundisho ya Uwongo yalikwisha nyemelea ndani ya kanisa hata nyakati za mitume.

C. Waaminio Umoja wa Mungu au Uimani wa Umoja wa Mungu
   1. Kundi hili lilithibitisha umoja wa Mungu kabisa na uungu wa Yesu. (Angalia maelezo Uk. 244-45.)
      a. Yuko Mungu mmoja tu (the *monarchia*)

b. “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” usielezee kama nafsi tofauti, lakini *aina* ya utendaji wa Mungu mmoja.
c. Yesu ni utimilifu wa Mungu uliovaa mwili.

2. Ilikuwa ni imani ya wakristo wengi katika zaidi sana karne ya tatu
3. Waalimu maarufu walikuwa Noetus, Praxeas na Sabelliius.

D. Karne ya Nne Hadi Sasa

1. Uimani wa Mungu mmoja inawezekana ilidumu kati ya makundi ya watu mbali mbali “wenye uasi” kutoka karne ya nne hadi Mihula/kipindi cha kati.
2. Wakati wa marejesho, Mchael Servetus (1511-53) alifundisha mfumo wa umoja wa Mungu na John Calvin Wakamchoma moto.
3. Emanue Sweedenborg (1698-1772) alifundisha mfumo wa Umoja wa Mungu, lakini baadhi ya mafundisho yake yalikuwa yasiyo na kadiri/kipimo au makali.
4. A. U. S. aliyekuwa mtumishi wa Presbyterian kwa jina John Miller aliandika kitabu katika mwaka 1876 kilichofundisha Umoja wa Mungu.
5. Mifano mingi bado haijagunduliwa na utafiti wa sasa, na bila shaka mengi zaidi bado kwetu hajulikani. (Tazama jedwali lifuatalo.)
6. Waaminio Umoja wa Mungu katika siku za sasa wameordheshwa katika miaka ya 1913-14.
   a. Wako mamilioni ya wafuasi leo.
   b. Kuna idadi kadhaa ya mashirika ya Umoja wa Mungu. (Angalia ukurasa wa 249-250.)

Maelezo: Waamini Umoja wa Mungu (Modalisim)

Waamini wa Umoja wa Mungu Katika Historia

Angalia: Hatuelewi umuhimu wote kuhusu au kuweka bayana mafundisho ya watu wote wafuatao (baada ya mitume), lakini inaonekana kwamba walishikilia Umoja wa Mungu hasa na utimilifu wa uungu wa Yesu Kristo ambao kwamba hawakuamini utatu.

Karne	**Wahusika**
1st	Kanisa la Mitume
2nd	Mababa wa Kimitume, pamoja na Clement wa Roma, Iganatus, Polycarp
3rd	Waaminio Umoja wa Mungu, pamoja na Praexas, Epigonous, Cleommenes, Sabellius Bila shaka maaskofu wa Kirumi Callistus na Zepyhrinus “Waamini wengi” katika siku za Tertullian
4th	Marcellus wa Ancyra, Photimus, Commodian, Priscillia, Sabllians
5th-15th	Sabellian, Priscillians, inawezekana pengine na baadhi ya “wakosaji”
16th	Michaeli Servetus, wapinzani wengi wa utatu, na baadhi ya Anabaptisti.
17th-18th	Baadhi ya Wabaptisti wa Uingereza, William Penn na baadhi ya Quakers, Emanuel Sweedenborg, Isaac Newton, Issac Watts
19th	Baadhi ya Makusanyiko Mapya ya Kiingereza, John Miller, Johna Cowes
20th	Wapentekoste wa Umoja wa Mungu, Wasabato baadhi, wakaresmaticki baadhi, baadhi ya Wabaptisti pamoja na Frank Stag.

Soma la 11
Utatu: Maelezo na Maendeleo Katika Historia

A. Maelezo:
   1. Kuna "Mungu mmoja katika nafsi tatu" (Utatu).
   2. Nafsi hizi zinalingana, umilele ulio sawa, na wote wa milele.
   3. Kuna hali/tabia tofauti kama ifuatavyo: Baba hakuzaliwa, Mwana amezaliwa, (aliumbwa) na Roho huendeleza (huvuvia)
   4. Kila nafsi hushiriki katika kazi ya mwingine.

B. Tatizo la Uimani ya Utatu
   1. Inaelekea utatu kuingliana (angalia nukuu uk.261-62)
   2. Inaelekea kupandana/kukingama na dhidi ya imani ya nafsi moja kuwa na umilele sawa, wakiukataa uungu wa Yesu.
   3. Inatumia maneno yasiyo msemo Ki-Biblia.
      a. Kamwe Biblia haikuwahi kutumia neno utatu.
      b. Biblia haikuwahi kutumia neno tatu kumhusu Mungu, isipokuwa 1 Yohana 5:17 inayosema "watatu hawa ni umoja."
      c. Biblia haikuwahi kutumia neno *tatu* kumwelezea Mungu.
      d. Biblia ya (King James) mara mbili imetumia neno nafsi kuhusiana na Mungu – Ayubu 13:8, inazungumzia upendeleo, na Waebrania 1:3, inazungumzia juu ya hali ya Mungu au badili.
      e. Mwana siyo nafsi ya pili, lakini aonekanaye, mfano wa Mungu Mwenyewe "nafsi" (Waebrania 1:3).
      f. Marejeo ya Wakatoliki wa msimamo wa kati na Waporestanti wanatambua kwamba waandishi wa ki-Biblia hawakufikiria wala kujieleza wenyewe katika hali za kiutatu.

C. Asili za Kipagani na Yafanayo nayo
   1. Utatu ulianzishwa na dini za kipagani za kale, hasa wale waliokuwa Wababeli na Misri.
   2. Utatu bado umeshikiliwa na dini za upagani leo, pamoja na Wahindu, Budha, na Taoism, ikionelewa kwamba ni chimbuko la upagani.
   3. Falsafa ya utatu ilionekana katika maandishi ya Pilato na ilikuwa inashikiliwa na Neo-Platisim (waliomfuata Pilato na imani yake), ambao ilikuwa maarufu sana kwa wanatheologia wa Kikristo.

D. Wa Apologists wa Kigiriki (130-180 B.K.)
   1. Waandishi wa Kikristo wa kwanza kufundisha wingi katika Mungu ni watetezi wa Kigiriki wa karne ya pili walioandika katika Kigiriki.
   2. Ajulikanaye sana ni Justin Myrty (mfia dini na mwanafalsafa wa kigiriki) aliyekuwa ameongoka katika ukristo.
   3. Walijaribu kupokea matamshi ya maneno mengi ya filosofia ya KigiriKi na mawazo ya Kikristo kuweza kupata kukubalika au kuwapata wapagani.
   4. Baadhi yao walianza kuzungumzia kuhusu Logos (neno katika Yohana 1) kama nafsi tofauti mbali na Baba, aliyeumbwa na Yeye na yuko chini Yake.
   5. Hawakuweka wazi Roho Mtakatifu kama nafsi ya tatu; lakini kwa hali Fulani walifanya hivyo, alionekana kuwa chini ya Baba pia.
   6. Mara ya kwanza kutajwa mfumo wa ubatizo wa aina tatu ulianza wakati huu, katika maandishi ya Justine kama mwaka wa 150 B. K
   7. Hawa waapologists walikuwa siyo wautatu katika ufahamu wao baadaye, lakini waaminio uungu mdogo wa Yesu.
   8. Theofilo alitumia neno la Kigiriki *triad* katika mwaka 189 B. K., walakini matumizi ya neno hilo haisemei utatu; maelezo kumhusu Mungu, Neno Lake, na hekima Yake.
   9. Inaonekana kwamba waamini wengi kimsingi bado ni waamini wa Umoja wa Mungu.

E. Waamininio Utatu wa Kwanza
    1. Tertulian (150-225) yeye ni baba wa imani ya utatu.
        a. Yeye alikuwa mwandishi wa kwanza kumwelezea Mungu kwa maneno ya Kilatini kuhusu *utatu* na *nafsi tatu* kama mwaka wa 200 BK.
        b. Alifundisha utatu wa kiuchumi, au utatu wa mafunuo, ambao utakoma katika umilele.
        c. Aliamini Mwana/Logos (nafsi ya pili) ilikuwa ni chini ya Baba (nafsi ya kwanza)
        d. Kwa nguvu alipinga waaminio umoja wa Mungu, ambaye alisema kuwa anaungwa mkono na waamini wengi.
    2. Maana ya Neno *nafsi*
        a. Awali, neno la Kilatini *nafsi (persona)* lingeweza kuwa utendaji au dhihirisho, lakini wautatu walilitumia kumaanisha kuwepo pekee au nafsi yenye kujitegemea.
        b. Neno la Kigiriki la nafsi *(hupostas au hypostasis)* kwa asili lilimaanisha hali, chimbuko, au dhihirisho binafsi, lakini baadaye maneno ya kigiriki na Kilatini yalionekana kama kushabihiana, yakimaanisha kama kiumbe kinacho jitegeemea.
    3. Origeni (alikufa 254) alitambulisha fundisho la Mwana wa milele na umilele wa uzao wa Mwana.
        a. Alijaribu kupinga filosofia ya Kigiriki na Kilatini
        b. Alisema kwamba Mwana alizaliwa tangu milele na milele alikuwa amezaliwa tangu milele.
        c. Alishikilia mwana kuwa mdogo kwa Baba katika kuwepo au asili, lakini waliendelea kuwa wote wako sawa.
    4. Hypolitus alimpinga Noetus katika Roma na kushutumu askofu wa Roma Callistus na Zepyrinus wa umoja wa Mungu.
    5. Novitian alikuwa ni mmoja wa kusisitiza Roho Mtakatifu kama nafsi ya tatu
    6. Kila mmoja wa hawa watu baadaye walitengwa au walitangazwa na kanisa lililokuwa limepangiliwa kwa mafundisho mbali mbali ya uwongo.
    7. Kama mwaka wa 300 utatu waliweka umoja wa Mungu kama imani iliyoaminiwa na wengi.

F. Baraza la Nikea la (325 BK.)
    1. Athanasius alifundisha kwamba Mwana ni nafsi pekee iliyo sawa, iliyo sawa milele, na uwezo sawa na Baba.
    2. Arius alifundisha kwamba Mwana aliumbwa kiumbe kilicho chini ya Baba.
    3. Uimani ya Arian-Athanasian ilisambaa katika Utawala wa Roma na kutishia umoja wake.
    4. Mtawala Costantine, aliyetumia Ukristo kudumisha mamlaka yake, aliitisha baraza kutatua mgawanyiko, na alilazimisha maamuzi.
    5. Wengi wa washiriki katika baraza walichanganyikiwa lakini walitaka amani.
    6. Matokeo yalikuwa:
        a. Kukataa wazi kwa Arius na kupitishwa kwa Athanasio.
        b. Tangazo rasmi la kwanza la kutokubaliana na umoja au Umoja wa Mungu.
        c. Tangazo la kwanza kuunga mkono uimani ya utatu.
    7. Angalia ukurasa wa 285 Imani ya awali wa Nikea.
        a. Inafundisha Mwana wa milele
        b. Haifundishi wazi wazi Roho Mtakatifu kama nafsi ya pili.

G. Baraza la Contantinapole (381 BK.
    1. Baada ya theolojia ya Nikea, kisiasa, na mapambano ya kijeshi yaliendelea kati ya Athaniso na –ARIAN. Kwa muda, ilionekana kama wa-Arian wanaweza kushinda, Wakiwa na kuungwa mkono kwa Utawala wa Costantius.
    2. Mabishano mapya yaliibuka juu ya uungu wa Roho Mtakatifu.

3. Baraza la Costantinople likasuluhisha maswala haya. Lilithibitisha/lilipitisha Baraza la Nikea, kutangaza kuwa RohoMtakatifu kuwa nafsi ya pili inayolingana, na kuongezea katika Ukiri wa Nikea.
4. Imani iliorejewa ni msemo wazi mpya wa utatu wa kisasa, na baraza likaweka hilo kama ushindi.
5. Nyongeza ya Imani ya Nikea ya Costantinople, *hotuba ya kuidhinisha,* lilipokelewa na Magharibi ila Mashariki.
    a. Othodox wa Kimashariki inasema kwamba Roho Mtakatifu anatoka kwa Baba tu.
    b. Ukatoliki wa ki-Roma na Uprosestant wanasema Roho Mtakatifu anatoka kwa Baba na kwa Mwana.

H. Imani ya Athaniso
1. Ukiri huu unajulikana sana katika matamshi ya utatu.
2. Ilipokelewa Mashariki baadaye katika miaka ya 400 BK. Au baadaye, lakini siyo na Athanasio, lakini wafuasi wa Augustino.
3. Angalia ukurasa wa 281-82 kwa maandishi ya ukiri.
4. Inaelezea kwamba kuamini utatu kulingana na maelezo yake ni lazima kwa wokovu.

I. Imani ya Mitume
1. Ukiri huu siyo wa asili wa kimitume.
2. Mfumo huu awali ulianzia Roma katika karne ya pili.
3. Haifundishi imani ya utatu, lakni unatumia lugha ya Kibiblia. (Angalia ukurasa 283)
4. Haufai kutumia kwa siku za leo
    a. Kiudanganyifu inazungumzia mamlaka ya kimitume.
    b. Haielezei maana kuu muhimu ya mafundisho yote, hasa katika nuru kwa mafundisho ya uwongo leo.
    c. Inafaa kurejea katika Maandiko yenyewe kwa ajili ya majumuisho ya mafundisho.
    d. Inatumika leo inaweza kutuhusisha na imani ya utatu.

Ufafanuzi na utambulisho: imani ya utatu, Wafuasi wa Kigiriki, Tertullian, Origen, kizazi cha milele, Athanasio, Arius, Baraza la Constatinople, Imani ya Nikea, Imani ya Athanasio, Imani ya Mitume.

Soma la 12
Imani ya Utatu – Tathmini

A. Maneno Yasiyo ya ki-Biblia
1. Ni hatari kutumia maneno yasiyo ya ki-Biblia matupu yasiyoendana na matamshi/maneno ya kibiblia lakini badala yake yanatambulisha wazo jipya.
2. *Nafsi moja* na *Nafsi nyingi*
    a. Nafsi humwekea Mungu kiwango kwa maana yetu ya kibinadamu
    b. Nafsi huelekeza kwenye uimani ya kwamba Mungu ni kama mmoja katika jeshi la mbinguni.
3. *Tatu* na *Utatu*
    a. Maneno haya yanaongoza katika imani ya kuamini utatu
    b. Maneno yote mawili yanaelezea namba moja tu katika uhusiano na Mungu.
4. Ingawaje waamini wa utatu wanakataa kuwa kuamini katika tatu, katika utendaji wao na mtazamo wao na maelezo yao yanalielekeza hilo.
5. Waamini wa utatu huwa wanaepuka majadiliano ya wenye busara na pingamizi la maandiko la mafundisho yao kwa kusema kwamba ni fumbo.

6. Waamini wa utatu wathibitisha uungu wa Yesu, lakini katika utendaji wa fundisho lao wanachepuka kutoka katika utimilifu wa uungu Wake na mabishano yao yanamshusha Yeye kuwa nafsi nyingine.

B. Kupingana
    1. Haiwezekani kwa Mungu kuwa nafsi tatu katika maana yoyote yenye busara na bado kuwa mmoja kabisa kama Maandiko yanavyotangaza.
    2. Imani ya utatu inajipinga yenyewe na inapingana na maandiko. (Angalia mifano ukurasa wa 293-98)

C. Mafundisho ya Umoja wa Mungu yanapingana na Imani ya Utatu.
    1. Kabisa Mungu ni mmoja, pasipo wingi wa nafsi.
    2. Baba Mwana na Roho Mtakatifu ni kazi tofauti zilizopangiliwa na Mungu, vyeo hivi vinaelezea kazi, madhihirisho, aina ya shughuli, namna ya madhihirisho ya Mungu mwenyewe, au mahusiano kwa wanadamu.
    3. Yesu kabisa ni uungu, kwa namna yoyote ile Yeye hawezi kuwa mdogo kwa mwingine yeyote.
    4. Wakati mtimilifu ulipowadia Mwana wa Mungu alizaliwa; neno *Mwana* inazungumzia kuutwaa mwili.
    5. Neno (Logos) siyo nafsi tofauti toka kwa Mungu, lakini ni nia ya Mungu, au Mungu akijidhihirisha Mwenyewe.
    6. Yesu ni jina kuu la Mungu lililodhihirishwa kwetu leo.
    7. Ubatizo wa maji unatendwa kwa jina la Yesu.
    8. Umoja wa Mungu siyo fumbo; fumbo la Mungu ni kuutwaa mwili, na limekwishafunuliwa.
    9. Tutaona uungu mmoja mkuu mbinguni: Yesu.

D. Mwisho Kuhusu Imani ya Utatu
    1. Fundisho hilo siyo la maneno ya kimaandiko, mawazo, wala awali kihistoria.
    2. Hayaongezi faida wazi kwa ujumbe wa Kikristo, badala yake huchepusha kutoka huko.
    3. Wastani wa waamini hawauelewi.
    4. Wa utatu wengi huwazia maneno ya Umoja wa Mungu.
    5. Swali rahisi litasaidia kuweka sawa hili swala: Tutaona wangapi mbinguni kwenye mamlaka – moja au tatu?
        a. Hatutawaona “watatu katika mmoja” aidha tutawaona watatu au mmoja.
        b. Kama jibu la mtu ni “tatu” basi waaminio utatu hamwamini Mungu mmoja katika hali yoyote yenye maana.
        c. Kama jibu ni “mmoja” basi huyo Mmoja ni nani? Kwa wazi ni Yesu. (Angalia IV-H.) Kama mtu ataelewa ukweli huu, basi ni wazi amepokea hali ya Umoja wa Mungu.
        d. Kama jibu ni “sijui” basi mtu huyu ana jambo dogo sana la Mungu anayetafuta kumtumikia. Je! Anayo mahusiano na nani aliye na uhusiano naye kumtumikia? Anaomba kwa nani? Anatarajia kukutana na nani?
    6. Kwa kupingana, Mafundisho ya Umoja wa Mungu ni ya kimaandiko na huleta mibaraka mingi. Ni ya lazima kwa kanisa. {Angalia XIII (13).}

Soma la 13
Tamati/Mwisho

Angalia ukurasa wa 298-306

E. Maelezo ya Fundisho la Umoja wa Mungu
   1. Yuko mmoja, Mungu asiyeoneka asiye na nafsi tofauti
   2. Yesu ni ukamilifu wa Uungu Aliyeuvaa mwili (Ndiyo kusema, majina na vyeo vya Uungu humwelezea Yeye.

F. Hitimisho la Fundisho la Umoja wa Mungu
   1. Mungu ni Mmoja (Kumbukubu la Torati. 6:4).
   2. Mungu ni Roho (Yohana 4:24).
   3. Mwana ni Mungu katika mwili (Luka 1:35; Wagalatia 4:4).
   4. Yesu ni uakamilifu wa Mungu katika mwili (Wakolosai 2:9).
   5. Yesu ni Baba katika mwili (Isaya 9:6; Yohana 10:30; 14:6-11).
   6. Yesu ni Roho Mtakatifu katika mwili (2 Wakorintho 3:17; Wagalatia 4:6).
   7. Ubatizo ni katika jina la Yesu (Matendo 2:38).

G. Umuhimu wa Fundisho la Umoja wa Mungu
   1. Biblia inalisizitizia
   2. Inafunua ukweli wa utambulisho wa Yesu.
   3. Inafanya nguvu ya jina la Yesu kuwepo kwetu.
   4. Linafundisha mfumo sahihi wa ubatizo.
   5. Inafundisha umuhimu wa kupokea Roho Mtakatifu, kwa kutaja, inamaanisha kumpokea Kristo.

D. Kuwashudia Wengine
   1. Tusiwashutumu, kusababisha uhasama, wasiwekwe kwenye kundi fulani.
   2. Lazima tuwaongoze wengine kwenye ukweli huu ili kurejesha fundisho la kimitume na nguvu.

H. Umuhumu wa Kuishi Maisha ya Kikristo
   1. Kufahamu umoja wa Mungu ni msingi wa kupata tukio la wokovu, kuabudu, na utakatifu (Marko 12:28-31; Yohana 17:3).
   2. Muumbaji wetu alifanyika Mwkozi wetu.
      a. Mungu Mwenyewe alikuja (2 Wakorintho 5:19)
      b. Mungu *Aliyetuambia* jinsi ya kuishi alikuja katika mwili kuleta ukombozi na kutu*onyesha* jinsi ya kuishi.
   3. Muumbaji-Mwokozi wetu pia ni Roho ikaayo ndani inayohuisha, hutakasa, na kututia nguvu. Ana*tuwezesha* kuishi kwa ajili Yake.
   4. Tumekamlika katika Yesu Kristo (Wakolosai 2:9-10). Katika Yeye tunao wokovu, ukombozi, uponyaji na ushindi.